OFISI YA MKUU WA MKOA WA KAGERA

TUPASHANE HABARI

KAGERA, KAZI AMANI NA MAENDELEO

21 JANUARI, 2016

# TUPASHANE HABARI

**YALIYOMO**

- ***Fedha za Elimu Bila Malipo zimewasili shuleni Mkoani Kagera***
- ***Utawala wafanya Kikao kazi***
- ***EFTA Wafungua Tawi Kagera***
- ***Jeshi la Zimamoto Latoa Elimu Manispaa ya Bukoba kwa shule za msingi***
- ***Jambo Bukoba Kuendesha Bonanza la Michezo***
- ***Mtumishi RS alazwa Muhimbili.***

*Tembelea Tovuti ya Mkoa*

*Www.kagera.gotz*

*Ukurasa wa Facebook*

*Kagera RS*

**NDANI YA JARIDA**


| | |
|---|---|
| EFTA Wafungua Tawi Kagera | 2 |
| Utawala wafanya Kikao Kazi | 2 |
| Fedha za Elimu Kagera | 3 |
| Jeshi la Zimamoto laelimisha Wananchi Bukoba | 4 |
| Jambo Bukoba Kuendesha Bonanza la Michezo | 4 |


## Fedha za Elimu Bure Mkoani Kagera Zawasili Shuleni

Mkoa wa Kagera tayari umepokea shilingi milioni 810,157,000/= kutekeleza sera ya elimu bure kwa shule za Msingi na Sekondari kutoka serikali kuu na tayari fedha hizo zimewekwa kwenye akaunti za shule zote za msingi 888 na sekondari 190 za serikali kwa kila Halmashauri katika Wilaya saba za Mkoa wa Kagera.

Hayo yalisemwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera Bw. Nassor Mnambila katika Mkutano na vyombo vya habari uliofanyika Januari 11, 2016 Katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera alipotoa ufafanuzi wa mgawanyo wa fedha zilizoletwa katika Mkoa mzima na jinsi zilivyogawiwa katika kila Halmashauri ya Wilaya kwa shule za Msingi na Sekondari kwa ajili ya kutekeleza Sera ya Elimu bila Malipo.

Akitoa ufafanuzi wa fedha zilizoletwa Mkoani Kagera Bw. Mnambila alisema shilingi 309,461,000/= zimepelekwa katika shule za msingi 888 ambapo shule 16 kati ya hizo.. ***Inaendelea Uk. 2***



***Mwanafunzi Akifanya Mazoezi Kwenye Maabara***

## Watumishi Sehemu ya Utawala Wafanya Kikaokazi

Sehemu ya Utawala na Rasilimali Watu Kilifanyika kikao cha watumishi wa sehemu hiyo tarehe 15 Januari, 2016 na kujadili mambo mbalimbali muhimu yanayohusu ustawi wa watumishi katika utumishi wa umma.

Katika kikao hicho ulitolewa ufafanuzi wa fomu ya maadili kipengele kwa kipengele kwa kuwakumbusha watumishi kufuata miiko na maadili ya utumishi na malengo ya serikali kwa kila mtumishi mmoja mmoja kusaini fomu hizo na kurejerea kiapo cha utumishi katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Aidha, katika kikao hicho watumishi walikumbushwa umuhimu wa kuwahi kazini ikiwa ni pamoja baadhi ya kada kukumbushwa utaratibu wa kufuata ili waweze kupandishwa vyeo katika utumishi.

Bw. Emily Ishengoma Afisa Utumishi aliwakumbusha watumishi wa sehemu ya utawala kujaza fomu za OPRAS ili kupima utendaji wao wa kazi.

Pia, katika kikao hicho ..***InaendeleaUk. 2***

**Inatoka Uk . 1**

***Kikao cha Watumishi Utawala***

yaliwasilishwa mapendekezo kuhusu usafiri kwa watumishi (basi la ofisi) kwa ajili ya kuwaleta watumishi kazini na kuwarudisha ambapo watumishi walipitia mapendekezo hayo na kutoa maoni yao kwa kamati husika ili iweze kufanya marekebisho.

Watumishi wa sehemu ya Utawala na Rasili-mali Watu waliazimia kuwa kikao hicho kiwe kinafanyika mara mbili kwa mwezi.

*"Tuwakumbuke Watumishi Wenzetu Katika sala na Dua Wanaopatiwa Matibabu Kwasasa Hasa Wale Waliolazwa Hospitali, Bi Sajida Mabale (Muhimbili) na Bw. Julius Samwel (Bugando) na wengineo wenye matatizo kiafya"*

# FURSA MPYA YA MIKOPO YA MASHINE KWA WAJASILIAMALI KATIKA UWEKEZAJI YAZINDULIWA RASMI MKOANI KAGERA

Equity for Tanzania (EFTA) wamefungua na kuzindua tawi jipya katika Manispaa ya Bukoba tarehe 15 Januari, 2016. Equity for Tanzania (EFTA) ni kampuni ya Kitanzania iliyoanzishwa mwaka 2004 na inajihusisha na utoaji wa huduma za mikopo ya mashine kwa wajasiriamali pasipo kuwa na sharti la kuhitaji dhamana kutoka kwa mkopaji.

**K**atika maeneo ambako EFTA wameshafungua Ofisi jumla ya watu wapato 170 wamejitokeza na kukopa mashine za kutengeneza mikate, mashine za kutotoresha vifaranga, magari ya kusafirishia bidhaa, mashine za kutengenezea sabuni. Aidha mikopo hutolewa kuanzia Tshs 20 mil hadi Tshs 200 mil.

**E**FTA pamaoja na kufungua tawi katika Mkoa wa Kagera ili kuvutia uwekezaji kwa wajasiliamali tayari wame-fungua matawi yao katika mikoa ya Kilimanjaro, Mwanza, Arusha, Morogoro pamoja na Mbeya.

**A**kizindua EFTA tawi la Bukoba Mkuu wa Mkoa Kagera Mhe. John Mongella alisema mikopo inayotolewa na EFTA ina manufaa makubwa kwa wajasiriamali kwa kuwa hakuna dhamana ya aina yoyote inayohitajika.

**"W**ananchi walio wengi wamekuwa wakikosa huduma za mikopo kutokana na kukosa dhamana kama nyumba na mashamba/viwanja, hivyo uzinduzi wa ofisi hii ya EFTA Mkoani Kagera inatoa fursa kubwa kwa wananchi hasa walio na shughuli za uzalishaji mali ili kujiendeleza zaidi kwa kukopa mashine za aina mbalimbali kutoka EFTA kulingana na mahitaji." Al-isistiza Mhe Mongella.

**P**ia Mhe. Mongella alisema Mkoa na Serikali kwa ujumla imekuwa ikisisitiza na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vidogo, vya kati na vikubwa kwa ajili kuongeza thamani mazao ya kilimo na mifugo na hatimaye kukuzaji ajira na pato la Mkoa na Taifa.

**I**fahamike kuwa viwanda bila mashine ni kazi bure, hivyo ni dhahili kuwa fursa hii imekuja wakati muafaka kwa kuwa changamoto kubwa na ya muda mrefu iliyokuwa ikiwakabili wajasiriamali walio wengi ni upatikanaji wa mitaji pamoja mashine za kisasa zinazoenda sambamba na ukuaji wa teknolojia.

**N**chini Tanzania zipo taasisi nyingi zinazojihusisha na utoaji wa mikopo mikubwa na midogo kwa mfumo wa kutoa pesa taslimu moja kwa moja kwa mlengwa. Hali hii imekuwa na changamoto kubwa ya wakopaji kutumia mikopo hiyo kinyume na malengo yaliyokusudiwa hivyo kupelekea kushindwa kulipa mikopo au kutolipa kwa wakati na hatimaye baadhi ya wakopaji kuuziwa mali zao.

**T**ofauti na taasisi hizo, EFTA wanatoa huduma za kipekee kwa kutoa mikopo ya mashine na sio pesa taslimu kwa wakopaji na huwalipa moja kwa moja wasambazaji/ watengenezaji wa mashine kulingana na mahitaji ya mteja. Riba ya mikopo ya EFTA ni asilimia 1.1% kwa mwezi sawa na asilimia 13.2% kwa mwaka ambapo makao makuu ya EFTA yapo Moshi mkoani Kilimanjaro.

**W**ananchi wa Mkoa wa Kagera wameombwa kuchangamkia fursa hiyo ili kupata kujiinua kiuchumi na kuingizia pato lao wenyewe na kukuza uchumi wa Mkoa na Taifa. EFTA tawi la Bukoba ofisi zao zipo mkabala na Soko Kuu la Bukoba katika mtaa wa Migeyo.

## Fedha za Elimu Bure Mkoani Kagera Zawasili Shuleni ....

*Inatoka Uk. 1*

....ni shule za wanafunzi wenye mahitaji maalum. Fedha hizo ni ruzuku ya uendeshaji (Capitation Grant) kwa kila shule ambapo kila mwanafunzi ametengewa shilingi 10,000/= kwa mwaka, na zitzkuwa zikitolewa kwa awamu kwa kila mwanafunzi kwa mwaka.

**V**ile vile zimetengwa fedha za chakula kwa shule maalum 16 za msingi katika Mkoa. Akitolea ufafanuzi wa shule maalum na shule za kawaida Bw. Mnambila alisema shule ya Kashalala iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ni ya kawaida na tayari imeishapokea shilingi 354,000/= kupitia Benki ya NMB Tawi la Kayanga.

**S**hule ya Msingi ni Mgeza Mseto ni shule maalum iliyopo katika Manispaa ya Bukoba nayo ipokea shilingi 7,728,000/= kupitia akaunti yake ya NMB Tawi la Bukoba, kati yake shilingi 3,042,000/= ni ruzuku ya uendeshaji na shilingi 7,386,000/= ni fedha ya chakula kwa wanafunzi waliopo katika shule hiyo.

**K**wa upande wa shule za Sekondari za Serikali Mkoa una jumla ya shule 190 kati ya hizo 17 ni za bweni na shule zote zimepewa fedha kwa ajili ya chakula shilingi 1,500/= kwa kutwa kwa kila mwanafunzi wa shule za bweni, na Serikali imetoa fedha za fidia za ada kwa shule za kutwa shilingi 20,000/= na shilingi 70,000/= kwa shule za bweni. Pia imetoa shilingi 25,000/= kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kama ruzuku ya uedeshaji.

**K**wa uthibitisho wa fedha kupokelewa shuleni Bw. Mnambila alitoa mfano wa shule ya kutwa ya Nemba iliyopo Wilayani Biharamulo kuwa tayari imepokea shilingi 630,000/= kwa ajili ya ada, shilingi 602,000/=kwa ajili ya ruzuku ya uendeshaji, ambapo shule hiyo imepokea shilingi 1,232,000/= kupitia akaunti yake ya NMB Tawi la Biharamulo.

**K**wa shule za bweni, shule ya Sekondari ya Rugambwa iliyopo Manispaa ya Bukoba imepokea shilingi 31,179,000/= kwa ajili ya chakula, shilingi 4,897,000/= kwa ajili ya fidia ya ada, na shilingi 1,535,000/= kwa ajili ya ruzuku ya uendeshaji, ambapo shule hiyo tayari imepokea shilingi 37,611,000/= kupitia akaunti yake ya NMB Tawi la Bukoba.

**Mwongozo wa Matumizi ya Fedha Kwa shule za Msingi, F**edha za ruzuku ya uendashaji zitumike kununulia vifaa vya kufundishia na kujifuzia na isiwe zaidi ya asilimia 30% ya fedha za ruzuku ya uendeshaji. Asilimia 30% ya fedha hizo pia itumike katika ukarabati mdogomdogo, asilimia 20% itumike katika mitihani na uendelezaji wawanafunzi na mwisho asilimia 10% ya fedha za ruzuku ya uendeshaji itumike katika mambo ya utawala shuleni.

**Shule za Sekondari,** Fidia ya ada ambayo serikali imetoa kwa kila shule badala ya wazazi kulipia itumike kugharamia mambo ya jumla ya uendeshaji wa Ofisi mfano vitambulisho, shajala, maandalio ya somo, ulinzi wa shule, madawa shuleni, uendeshaji wa taaluma (chaki, manila, karatasi, michezo, mitihani ya uendelezaji wa wanafunzi mfano majaribio ya wiki, na mitihani ya moko).

**Wito,** Katibu Tawala Bw. Mnambila alitoa wito kwa Walimu Wakuu wa shule za Msingi na Wakuu wa shule za Sekondari kuzingatia miongozo ya matumizi ya fedha hizo kwa kufuata maelekezo ya serikali na kuacha kuyadharau kama vile baadhi yao ambao bado hawataki kuyafuata maelekezo hayo. Hivyo, alitangaza kumvua madaraka Mkuu wa wa shule ya Sekondari Bilele Bw. Siasa Phocus ambaye ameendelea kutoa fomu zinazoonesha gharama za uchangiaji kwa wazazi wa wanafunzi wanaojiunga kidato cha kwanza na kusema kuwa maelekezo ya serikali hayatambui.

**Mgawanyo wa Fedha kwa kila Halmashauri**

**K**wa shule za Sekondari Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo imepokea shilingi 76,525,000/=, Bukoba shilingi 56,462,000/=, Bukoba Manispaa shilingi 122,597,000/=, Karagwe shilingi 39,639,000/=, Kyerwa shilingi 21,403,000/=, Missenyi shilingi 29, 833,000/=, Muleba shilingi 93,757,000/=, Ngara shilingi 60,480,000/=

**Aidha, k**wa shule za Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo imepokea shilingi 43,161,000/=, Bukoba shilingi 36,704,000/=, Manispaa ya Bukoba shilingi 27,385,000/=, Karagwe shilingi 37,515,000/=, Kyerwa shilingi 37,967,000/=, Missenyi shilingi 20,115,000/=, Muleba shilingi 69,219,000/=, Ngara shilingi 37,397,000/=

## JESHI LA ZIMAMOTO MANISPAA YA BUKOBA LATOA ELIMU JUU YA MAJANGA YA MOTO.

Jeshi la Zima moto katika Manispaa ya Bukoba limeendesha mafunzo na kutoa elimu kwa wananchi wa Bukoba juu ya kujikinga na na kupambana na majanga ya moto.

**M**afunzo hayo yaliendeshwa na Jeshi hilo tarehe 15/01/2016 katika viwanja vya Gymkhana Manispaa ya Bukoba na kuhudhuriwa na wananchi kutoka katika viunga vya Manispaa ya Bukoba.

**A**kifungua mafunzo hayo Mkuu wa Wilaya ya Bukoba Mhe. Jackson Msome aliwasistiza wananchi kulitambua Jeshi la Zimamoto na kuacha kusubiri wakati wa majanga tu ndo wanalikumbuka Jeshi hilo bali watumie muda wao pia kulitembelea na kupata elimu juu ya majanga ya moto.

**M**aafisa wa Jeshi hilo walitoa elimu kwa wananchi jinsi ya kukabiliana na majanga ya moto kwa kutumia vifaa mbalimbali vya kuzimia moto ikiwa ni pamoja na kutumia maji na kutambua aina ya moto kabla ya kuzimwa.

**E**limu ya kutoa taarifa mapema kwa Jeshi la Zimamoto pale janga la moto linapotokea ilitolewa na jinsi ya kujiandaa kukabiliana na moto kwa kutumia vifaa vidogovidogo ambavyo vinakuwepo katika majengo kabla ya Jeshi hilo kuwasili katika eneo husika.

**A**idha wananchi walikumbushwa kuvifanyia marekebisho vifaa vya kuzimia moto kama mitungi ya kuzima moto mara baada ya muda ulioelekezwa kifaa hicho kutumika kuisha.

**T**aasisi za serikali na zisizokuwa za serikali na wananchi binafsi walistizwa umuhimu wa kupata mafunzo katika maeneo yao na watumishi wao ili kuhakikisha kila muhusika katika eneo alilopo anajua hatua muhimu na za awali wakati janga la moto linapojitokeza.

**V**ile Jeshi hilo limewakumbusha wananchi kuwaalika kufanyiwa ukaguzi wamajengo yao kama yanakidhi au yapo salaama kuepukana na majanga ya moto.

## JAMBO BUKOBA KUENDESHA BONANZA LA MICHEZO KATIKA MANISPAA YA BUKOBA KWA SHULE ZA MSINGI

Shirika la Jambo Bukoba lisilo la serikali linalojihusisha na masuala ya michezo mkoani Kagera linatarajia kufanya bonanza la michezo kwa shule za msingi mkoani Kagera linalotarajiwa kufanyika tarehe 29 Januari, 2016 katika Manispaa ya Bukoba.

**B**onanza hilo litahusisha wananfunzi wanamichezo 240 kutoka katika shule za msingi nane, wanafunzi 30 kila shule moja kutoka kila Halamashauri, wanafunzi hao watakuwa wavulana 15 na wasichana 15 watakaowakilisha kila Halmashauri wakiwa na walimu wao wa michezo.

**S**hirika hilo ambalo mwazilishi wake ni Bwana Clemence N. Mulokozi ambaye Baba yake alikuwa mwenyeji wa Ishozi Wilayani Missenyi na mama yake ni Mjeurumani kabla ya kufanyika bonanza la michezoinatarajiwa kufanya kongamano tarehe 27.01.2016 na walimu wa michezo wawili wawili kutoka katika kila Halmashauri.

**A**idha tarehe 29.01.2016 pia utafanyika mkutano wa tathimini juu ya shughuli za Jambo Bukoba utakaowahusisha walimu na wadau wa michezo wakiwemo Wakurugenzi watendaji wa Halmashauri ili kujua mafanikio yaliyofikiwa china ya Jambo Bukoba na changamoto pia zilizojitokeza mwaka 2015 na jinsi ya kuzitatua changamoto hizo.

**S**hule zitakazoshiriki katika bonanza hilo zilipatikana kutoka kila Halmashauri kwa kuendesha mabonanza ya Wilaya na shule washindi ndiyo watakao shiriki kuwakilisha shule nyingine kwenye Wilaya. Shule hizo ni Kaagya (Halmashauri ya Wilaya Bukoba), Iteera (Kyerwa), Ibuga (Muleba), Mafumbo (Bukoba Manispaa), Murusagamba (Ngara), Mwemagea (Missenyi), na Maguge (Karagwe).

**W**ashindi watakaopatikana katika mashindano ya bonanza hilo watazawadiwa shilingi 4,000,000/= kila shule na fedha hizo zitatumika katika kuimarisha miundombinu ya shule husika kama kujenga matundu ya vyoo, kukarabati madarasa na ofisi za walimu kwa kushirikiana na jamii ya eneo husika.

**A**idha Bw. Steven Gonzaga Meneja wa Shirika hilo alisema katika bonanza hilo la michezo wanatarajiwa wageni kutoka nchini Ujerumani na Kenya marafiki wa shirika hilo ambao watakuja kushiriki katika bonanza hilo na kujifunza